

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

133

KISWAHILI

MUDA: SAA 2.00

JUMANNE 03 DISEMBA, 2019 MCHANA

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBDARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 12 zenyé maandishi

Ukurasa wa **1** kati ya **12**

SEHEMU A: (Alama 15)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Soma **mtoto** wa kike,
Soma usishawishike,
Soma nyadhifa ushike,
Soma nakutegemea,

Soma usitetereke,
hadi mwishowe ufile,
nchi hii utumike,
Soma mtoto wa kike.

Soma na ufundishike,
Soma nami niridhike,
Soma kisha unizike,
Soma nakutegemea,

na vikwazo uviruke,
moyo nisisononeke,
mahali **pema** niweke,
Soma mtoto wa kike.

Soma usirukeruke,
Soma yote ukumbuke,
Soma usirubunike,
Soma nakutegemea,

bongo zako zichemke,
masomo yasiponyoke,
mwanangu usipotoke,
Soma mtoto wa kike.

Soma usipaparike,
Soma usifedheheke,
Soma ili nitukuke,
Soma nakutegemea,

raha zina muda wake,
wenzangu wasinicheke,
heshima nami niweke,
Soma mtoto wa kike.

1. Maswali

- a) Bainisha nasaha mbili (2) anazozitoa mshairi kwa mtoto wa kike.

Nambari ya Mtahiniwa _____

- b) Eleza faida inayoweza kupatikana kwa jamii na mzazi endapo mtoto wa kike atapata elimu.

- c) Andika kichwa cha shairi hili kwa maneno yasiyozidi matano (5).

- d) Mshairi amekusudia kutoa ujumbe gani kwa jamii yake?

- e) Andika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari.

NENO	KINYUME

2. Fupisha shairi ulilolisoma hapo juu kwa **aya moja (1)** yenye maneno yasiyozidi ishirini na tano (25).

SEHEMU B: (Alama 40)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii. Swali la sita (6) ni la lazima.

3. a) Taja aina za sentensi zifuatazo:

i) Watoto wanaruka juu na chini.

ii) Kondoo aliyenunuliwa jana amechinjwa leo asubuhi.

iii) Tungelisoma kwa bidii hakika tungelifaalu mitihani yetu.

- b) Tunga sentensi moja kwa kila aina ya kiunganishi kifuatacho:

i. Kiunganishi linganishi

ii. Kiunganishi nyongeza

4. a) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

i) Tukilima tutavuna mazao mengi.

ii) Abasi si kijana mzuri.

iii) Jogoo amewika mara mbili.

b) Kwa kutumia mifano eleza maana ya istilahi zifuatazo:

i. Kishazi

ii. Sentensi

5. a) Eleza taratibu tatu (3) za kufanya mdahalo.

i)

ii)

iii)

b) i) Nini maana ya taarifa?

- ii) Taja sifa mbili (2) za taarifa.

6. a) Uliza maswali yafuatayo kwa Kiswahili.

- i) How many nails do you have in your fingers?

- ii) Which colour do you prefer, brown or purple?

- iii) Who is the President of this country?

- b) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

- i) 80,914

- ii) 32,500,500

7. a) Kiunguja na Kipemba ni miongoni mwa lahaja za lugha ya Kiswahili. Andika lahaja nyengine tatu (3) za lugha hiyo.

i) _____
ii) _____
iii) _____

- b) Fafanua kwa kutumia mifano mambo mawili (2) yanayotofautisha lahaja moja na nyengine.

i) _____

ii) _____

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.

8. Tunga hadithi fupi ya kusimua inayokubaliana na methali isemayo "Mtaka nyingi nasaba hupata mwangi msiba"

Nambari ya Mtahiniwa _____

9. Andika beti tatu (3) za wimbo wa Kiswahili unaokemea maovu yaliyomo katika jamii yako.

Nambari ya Mtahiniwa _____

10. a) Eleza mambo matatu (3) yanayotofautisha mashairi ya kimapokeo na ya kimamboleo.

i) _____

ii) _____

iii) _____

b) Tegua vitendawili vifuatavyo:-

i) Nina mti wangu kila nikiukata haukatiki.

ii) Ninampiga mwanangu kila siku lakini hasikii.

SEHEMU D: (Alama 15)

UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

11. Tunga Insha ya maneno kati ya 120 – 130 kuhusu “Umuhimu wa vyombo vyahabari”.

Nambari ya Mtahiniwa _____

12. Jaalia wewe ni Maulid Ussi Mussa unayeishi Mapambazuko, umefiwa na mtoto wako anayeitwa Zakaria Ussi Mussa. Andika tangazo la kifo kuwaarifu watoto wako Farida Ussi Mussa wa Uweleni Pemba, Hassan Ussi Mussa wa Mahonda, Rashida Ussi Mussa wa Mtwara, pamoja na ndugu, jamaa, marafiki na wengineo.

Nambari ya Mtahiniwa _____

Ukurasa wa **12** kati ya **12**